tax justice network

policy forum

Kielezo cha Usiri wa Fedha 2018

Utangulizi

Usiri wa Fedha unaelezwa kama hali inayojitokeza pale ambapo chombo kinachokubalika kisheria mfano taasisi au kampuni kinakataa kushirikisha taarifa zake za kifedha na mamlaka halali kama vile Mamlaka ya Mapato, mamlaka ya Usalama na kadhalika. Usiri wa fedha unaweza kuwa katika ngazi za siri za benki, siri za kampuni, au kutokutoa ushirikiano.

Kielezo cha Usiri wa Fedha (FSI) 2018 kimepanga katika safu nchi 112 (zilizopo kisheria) kufuatana na usiri wao na kiwango cha ushiriki wao katika shughuli za kifedha zinazofanyika kandokando mwa fukwe za bahari. Mpangilio kisafu ambao haufungamani na upande wowote kisiasa, ni chombo cha kuwezesha uelewa wa usiri wa kifedha ulimwenguni, ukwepaji wa kodi au mamlaka za usiri, na usafirishaji haramu wa fedha au utoroshaji wa fedha. Biashara ovu ya kiulimwengu imeanza na inahusisha benki kubwa ulimwenguni, taratibu za kisheria, makampuni ya uhasibu na wabobezi katika huduma hii ambayo huunda na kutafuta masoko kwa wateja wao wakwepa kodi na wakwepa taratibu za kisheria. Katika kuwafichia siri hiyo, dunia ya magwiji wa usiri huo wa ufukweni hupotosha na kughilibu masoko na uwekezaji na kuyafanya yasiwe na ufanisi. Dunia hiyo ya magwiji wa usiri hutengeneza kambi ya wavunja sheria kwa maovu mengi ikiwa ni pamoja na ulaghai, udanganyifu wa kodi, ukwepaji wa kanuni za kifedha, ubadhirifu, uhujumu uchumi / ufisadi, utoaji na upokeaji hongo, utakatishaji fedha na mengine mengi. FSI inaonyesha kwamba wabobezi zaidi katika usiri wa fedha duniani siyo visiwa vidogo vilivyozungukwa na minazi kama wengi wanavyodhani, bali ni baadhi ya nchi kubwa na tajiri zaidi duniani. Matokeo ya jumla yanaonyesha kuwa Slovenia ni nchi yenye usiri mdogo zaidi wa kifedha ikiwa na asilimia 41.83 wakati Vanuatu ni nchi yenye usiri mkubwa zaidi ikiwa na asilimia 88.54.

Matokeo Nchini Tanzania

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata asilimia 73 ya usiri pamoja na kuwa na sera za kuvutia kuhusu usiri, ni siku za hivi karibuni tu kwamba shughuli za nchini zimechunguzwa na kuwekwa wazi.



Uwekezaji wa Kifedha

Kufuatia kwa benki kuu kufilisi benki karibu tano nchini, imedhihirika kuwa Serikali inaunga mkono kampeni dhidi ya utakatishaji fedha, lakini imeendelea na msimamo wake wa kuweka siri taarifa kuhusu mmiliki wa mali hizo, hadi pale itakapopelekewa hati kamili kimaandishi ya uombwaji wa taarifa hizo.

Baadhi ya Wachina na Wahindi wanaichukulia Tanzania kama nchi nzuri ya kupeleka mali zao kutokana na usiri huo.

Ingawa sheria za kodi zimekuwa zinavutia siku zote kwa uwekezaji, ni siku za hivi karibuni tu ambapo Tanzania imeonekana kuwa kivutio kama nchi ya kisiri. Pamoja na kwamba sheria zipo, kuna udhaifu katika utekelezaji wa uhakiki unaofanywa na benki unaopaswa kuzingatia haki na usahihi.



Mnufaika wa Umiliki Katika Viwanda vya Uziduaji

Viwanda vya uziduaji vimetiwa kiwingu cha usiri na rushwa hadi kupelekea kwenye kashfa. Hivi karibuni, Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Acacia yenye makao yake makuu nchini uingereza ilionekana imekuwa ikitamka chini ya kiwango halisi cha madeni ya kodi inayodaiwa na Tanzania. Wakati wa Kilele cha Mkutano Dhidi ya Rushwa uliofanyika mwaka 2016 mwezi mei nchini Uingereza, serikali iliahidi kwamba taarifa za mnufaika wa umiliki wa makampuni yaliyowekeza katika viwanda vya uziduaji zitawekwa wazi kwa umma. Lakini mfumo wa kisheria kuhusu mnufaika wa umiliki haujakamilika kwani kwa viwanda vya uziduaji (madini, mafuta na gesi) makampuni yanatakiwa yachapishe majina ya wamiliki wao chini ya Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Viwanda vya Uziduaji ya mwaka 2015; hata hivyo hakuna kanuni zozote zilizoandaliwa kwa utekelezaji wake. Hata hivyo, kwa kupitia Mpango wa Uwazi katika Viwanda vya Uziduaji Tanzania (TEITI) serikali imejiunga na nchi nyingine katika kutambua wanufaika wa umiliki wa makampuni ya uziduaji yanayofanya kazi chini ya himaya yake; uwekaji wazi wa wanufaika wa umiliki ni lazima kisheria kwa nchi zinazotekeleza mkataba wa EITI kuanzia mwaka 2020. Hivi sasa, wanakamati wa TEITI wamekubaliana taratibu na hatua za kutekeleza uwekaji wazi wa mnufaika wa umiliki, ikiwa ni pamoja na kuanzisha uyakinifu wa kilele cha juu cha asilimia 1 ya kitega uchumi, kwa uwekwaji wazi wa mnufaika wa umiliki na kuandaa regista kuu ya kutunza taarifa kutoka makampuni ya uziduaji. Hii ni ishara nzuri kwa siku zijazo.

Mapendekezo

- Utengenezaji wa regista ya umma ya wanufaika wa umiliki wa makampuni.
- Hatua za hivi karibuni za kuunda sekta ya kisasa ya fedha ziambatane na nia ya dhati ya kufikia uwazi wa kisheria na kifedha.
- Kupambana moja kwa moja dhidi ya usiri wa kifedha ufukweni na miundo mbinu ya kidunia inayoiunda.
- Kutambua na kuzikwepa kadiri inavyowezekana mamlaka ambazo zimekumbatia na kufanya usiri wa ufukweni kuwa biashara yao.

policy forum

Contact us at:
Plot 14, Sembeti Road | Mikocheni B
P.O. Box 38486 | Dar es Salaam, Tanzania
Phone: +255 22 2780200 | Mobile: + 255 782317434
Email: info@policyforum.or.tz | Website: www.policyforum.or.tz